**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**

**SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni Taasisi inayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 132 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kutekeleza Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995.

Mojawapo ya jukumu la taasisi hii ni kuchunguza tabia na mienendo ya kiongozi wa umma yeyote kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yanazingatiwa.

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inatarajia kuwafikisha mbele ya Baraza la Maadili viongozi wawili kwa tuhuma za ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Viongozi hao ni Mhe. Onesmo Mpuya Buswelu ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, mkoa wa Katavi na Mhe. Yusuph Hamisi Kitumbo Diwani wa Kata ya Cheyo Halmashauri ya Manispaa Tabora Mkoa wa Tabora.

Baraza la Maadili linatarajia kufanya kikao cha uchunguzi wa kina wa malalamiko kwa mujibu wa kanuni ya 11 ya Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma (Mwenendo wa Uchunguzi wa Malalamiko katika Baraza la Maadili), 2017.

Kikao hicho cha uchunguzi kitafanyika kuanzia saa 3:00 asubuhi tarehe 4 na 7 Juni, 2024 jijini Dodoma katika ukumbi wa mikutano uliopo katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Aidha, wananchi wote mnaalikwa kuhudhuria katika kikao hicho muhimu.

..........................................

Jaji (Mst.) Sivangilwa S. Mwangesi

**Kamishna wa Maadili**

3 Juni, 2024